# SHERIA YA UVUVI NAM. 8 YA 1988

## SHERIA NDOGO NDOGO ZA USIMAMIZI WA ENEO LA HIFADHI YA GHUBA YA MENAI ZANZIBAR (CHINI YA KIFUNGU CHA 32)

Katika kutekeleza uwezo niliopewa chini ya kifungu cha 32 cha Sheria ya Uvuvi Nam. 8 ya 1988, MIMI, BURHAN SAADAT HAJI, Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira naweka sheria ndogo ndogo zifuatazo:

### SEHEMU YA KWANZA: UTANGULIZI

*Jina na kuanza kutumika*

**1.** Sheria hizi ndogo ndogo zitajulikana kuwa ni sheria ndogo ndogo za usimamizi wa maeneo ya hifadhi za bahari Zanzibar za mwaka 2009 na zitaanza kutumika mara baada ya kusainiwa na Waziri.

*Matumizi*

**2.** Sheria hizi ndogo ndogo zitatumika katika maeneo yote ya hifadhi za bahari Zanzibar

*Ufafanuzi*

**3.** Kwa madhumini ya sheria hizi ndogo ndogo, isipokuwa kama itahitajika vyenginevyo:-

"**Baruti**" maana yake ni bomu au mlipuko wa bomu unaoweza kusababisha uharibikaji au ubomoaji wa mazingira ya papo hapo, kwa kuua viumbe vilivyopo kwenye sehemu ya mlipuko huo.

"**Bunduki ya baharini**" maana yake ni kifaa au zana iliyotengenezwa kwa namna ya kusukuma msumari au kitu kinachofanana nao ambayo inatumika katika kuvulia na inajumuisha mchinji.

"**Chombo cha Uvuvi cha Zanzibar**" maana yake ni chombo kilichoandikishwa au kilichokatiwa leseni kwa mujibu wa kanuni kuu ya uvuvi Zanzibar ya mwaka 1993.

"**Dago**" Ni kukaa kambi kwa ajli ya kazi za uvuvi

"**Eneo la Hifadhi**" maana yake ni eneo la hifadhi ya bahari lililoanzishwa kwa mujibu wa sheria za uvuvi za Zanzibar.

"**Juya**" maana yake ni mtego wa uvuvi uliotengenezwa kwa nyavu yenye macho yasiozidi inchi 3 ambao huvuliwa kwa kuzungusha na kuburura chini ya bahari na hutegwa pembezoni mwa mafungu, fukwe, visiwa vidogo vidogo, kwenye ghuba, au sehemu ambazo samaki huzaliana pia inajumuisha gole, kigumi, na chavu.

"**Kamati ya uvuvi**" maana yake ni Kamati ya uvuvi iliyoundwa katika kijiji kilichoko nje ya eneo la hifadhi ya bahari Zanzibar.

"**Kamati ya uvuvi ya eneo**" maana yake ni Kamati ya uvuvi iliyoundwa katika kijiji kilichoko ndani ya eneo la hifadhi ya bahari Zanzibar.

"**Kijiji**" maana yake ni kijiji au shehia iliyoko nje au ndani ya eneo la hifadhi ya bahari ambamo kamati ya uvuvi imeundwa.

"**Mchinji**" maana yake ni msumari ambao hufungwa mpira nyuma na hutumika kwa kuvulia.

"**Mkurugenzi**" maana yake ni Mkurugenzi wa Uvuvi Zanzibar.

"**Mtando**" maana yake ni mtego wa nyavu unaotegwa kwa kuzungusha.

"**Mvuvi**" maana yake ni mtu yoyote mwenye leseni halali ya uvuvi iliyotolewa kwa mujibu wa sheria za uvuvi Zanzibar.

"**Tumbawe**" maana yake ni jiwe liliyopo baharini ambalo samaki na viumbe vyengine vya baharini hutumia kwa mazalio, malisho, na hifadhi yao.

"**Sumu**" maana yake ni madawa yanayotokana na viwanda au sehemu yoyote ya mti yanayoweza kulewesha au kuua viumbe vya baharini na inajumuisha utupa, ngwira, madawa ya mifugo na madawa ya kilimo.

"**Chau**" maana yake ni sehemu ya eneo la maji kupwa na kujaa iliyozikwa makumbi kwa ajili ya usumba.

## SEHEMU YA PILI: MAKATAZO, MAKOSA NA ADHABU

*Marufuku kutumia au kuwa na zana zilizokatazwa*

**4.** (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kutumia au kuwa na Juya, Bunduki Mtando, sumu itokanayo na madawa ya viwandani, baruti, nyavu yenye macho chini ya inchi mbili, nyavu za utari au nyavu nyengine yoyote ya kukokota katika eneo la hifadhi.

(2*) Mtu yeyote atakae kiuka amri ya kifungu hiki atakuwa ni mkosa na akipatikana na hatia ataadhibiwa kwa mujibu wa sheria mama ya uvuvi.*

*Marufuku kuwanayo au kutumia gesi kwa kazi za uvuvi*

**5.** (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuwanayo au kutumia gesi kwa kazi za uvuvi katika eneo la hifadhi.

*(2) Mtu yeyote atakae kiuka amri ya kifungu hiki na akipatikana na hatia ataadhibiwa kama ifuatavyo:-*

*(a) kwa kosa la mara ya kwanza watu waliohusika ndani ya chombo kimoja watatozwa faini isiyopungua shilingi 200,000/= na isiyozidi shilingi 500,000/=*

*(b) kwa kosa la mara ya pili na linaloendelea adhabu itakua kama ilivyo sehemu ya (a) hapo juu pamoja na kutaifishwa vifaa vyake.*

*Marufuku kuwanayo au kutumia sumu kwa kazi za uvuvi*

**6.** (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kutumia au kuwanayo sumu itokanayo na miti katika eneo la hifadhi.

*(2) Mtu yeyote atakae kiuka amri ya kifungu hiki na akipatikana na hatia ataadhibiwa kama ifuatavyo:-*

*(a) kwa kosa la mara ya kwanza atatozwa faini si chini ya shilingi 30,000/= na si zaidi ya shilingi 50,000/=*

*(b) kwa kosa la mara ya pili na linaloendelea atatozwa faini si chini ya shilingi 50,000/= na isiyozidi shilingi 100,000/=.*

*Marufuku kupanda mwani katika eneo lililokatazwa*

**7.** (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kupanda mwani, katika eneo la kupitishia Vyombo au sehemu ya kuegeshea vyombo vya uvuvi.

*(2) Mtu yeyote atakae kiuka amri ya kifungu hiki na akipatikana na hatia ataadhibiwa kama ifuatavyo:-*

*(a) kwa kosa la mara ya kwanza atapewa onyo la maandishi kutoka kwa kamati ya uvuvi ya eneo husika pamoja na kuondosha mwani wake.*

*(b) kwa kosa la mara ya pili na linaloendelea atatozwa faini si chini ya shilingi 10,000/= na isiyozidi shilingi 20,000/= pamoja na kuondosha mwani wake.*

*Marufuku kuharibu mwani, kufanya uvuvi au kuweka chombo katika shamba la mwani*

**8.** (1) Ni marufuku kwa mtu yoyote kuiba mwani, kuharibu shamba la mwani kwa namna yoyote ile, kufanya kazi za uvuvi katika shamba ya mwani, kuweka nanga au chombo cha uvuvi katika shamba la mwani liliyomo kwenye eneo la hifadhi.

*(2) Mtu yeyote atakae kiuka amri ya kifungu hiki na akipatikana na hatia atatozwa faini si chini ya shilingi 50,000/= na isiyozidi shilingi 70,000/= pamoja na kurejesha gharama za uharibifu aliofanya.*

*Marufuku kuharibu matumbawe*

**9.** (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuharibu au kuchukua matumbawe kwa madhumuni yoyote yale isipokuwa kwa ruhusa maalum iliyotolewa na Mkurugenzi wa Uvuvi.

*(2) Mtu yeyote atakae kiuka amri ya kifungu hiki na akipatikana na hatia atatozwa faini si chini ya shilingi 200,000/= na isiyozidi shilingi 500,000/=.*

*Marufuku kuchimba mchanga pepmbezoni mwa fukwe*

10. (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuchimba mchanga pembezoni mwa fukwe, mafungu au ndani ya bahari kwa ajili ya kazi zozote

*(2) Mtu yeyote atakae kiuka amri ya kifungu hiki na akipatikana na hatia atatozwa faini si chini ya shilingi 50,000/= na isiyozidi shilingi 100,000/= pamoja na kurejesha mchanga aliouchukua.*

*Marufuku kuchimba au kuvunja mawe pembezoni mwa fukwe*

11. (1) Ni marufuku kwa mtu yoyote kuchimba, kugonga au kuvunja mawe sehemu ya fukwe au kwenye magoma ndani ya eneo la hifadhi kwa matumizi yoyote.

*(2) Mtu yeyote atakae kiuka amri ya kifungu hiki na akipatikana na hatia atatozwa faini si chini ya shilingi 50,000/= na isiyozidi shilingi 500,000/= pamoja na kurejesha mawe aliouchukua*

*Marufuku kuvua mazao ya baharini yaliyofungiwa*

12. (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuvua, kuokota au kuchokoa zao lolote la baharini ambalo limefungiwa kwa mujibu wa maamuzi ya kamati ya uvuvi ya eneo katika kijiji husika.

*(2) Mtu yeyote atakae kiuka amri ya kifungu hiki na akipatikana na hatia ataadhibiwa kama ifuatavyo:-*

*(a) kwa kosa la mara ya kwanza atapewa onyo la maandishi kutoka kwa kamati ya uvuvi ya eneo husika na uongozi wa sheha pamoja na kunyang'anywa mazao hao.*
*(b) kwa kosa la mara ya pili atatozwa faini si chini ya shilingi 50,000/= na isiyozidi shilingi 100,000/= pamoja na kutaifishwa mazao hayo.*
*(c) kwa kosa la mara ya tatu na linaloendelea atafikishwa mahakamani kwa mujibu wa sheria mama ya uvuvi ya Zanzibar.*

(3) Kutakuwa na ufungaji wa uvuvi kwa mazao ya baharini kama vile pweza, samaki, makombe na majongoo kwa kipindi na maeneo maalum ndani ya eneo la hifadhi. Muda wa ufungaji utaamuliwa na Kamati ya uvuvi ya eneo ya kijiji husika na utakuwa si zaidi mara mbili kwa mwaka na si zaidi ya miezi miwili kwa kipindi kimoja.

*Marufuku kuharibu*

13. (1) Ni marufuku kwa mtu yoyote kuondosha au kuharibu mitego ya

*au kuondosha mitego ya uvuvi*

uvuvi iliyotegwa kwa halali ndani ya eneo la hifadhi bila ya ruhusa ya mhusika.

(2) *Mtu yeyote atakae kiuka amri ya kifungu hiki na akipatikana na hatia ataadhibiwa kama ifuatavyo:-*

*(a) kwa kosa la mara ya kwanza atapewa onyo la maandishi kutoka kwa kamati ya uvuvi ya eneo husika pamoja na kulipa gharama uharibifu wa mitego.*
*(b) kwa kosa la mara ya pili na linaloendelea atatozwa faini si chini ya shilingi 100,000/= na isiyozidi shilingi 200,000/= pamoja na kulipa gharama za uharibifu wa mitego.*

*Marufuku kuharibu maeneo ya kufugia samaki*

14. (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuharibu maeneo ya kufugia samaki na mazao mengine ya baharini katika eneo la hifadhi.

*(2) Mtu yeyote atakae kiuka amri ya kifungu hiki na akipatikana na hatia atatozwa faini si chini ya shilingi 50,000/= na isiyozidi shilingi 100,000/= pamoja na kurejesha gharama za uharibifu aliofanya.*

*Marufuku kuharibu vyau*

15. (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuharibu vyau kwa ajili ya kutafuta chambo au kwa namna nyinginezo yoyote.

(2) *Mtu yeyote atakae kiuka amri ya kifungu hiki na akipatikana na hatia ataadhibiwa kama ifuatavyo:-*

*(a) kwa kosa la mara ya kwanza atapewa onyo la maandishi kutoka kwa kamati ya uvuvi ya eneo husika pamoja na kulipa gharama uharibifu wa chau.*
*(b) kwa kosa la mara ya pili na linaloendelea atatozwa faini si chini ya shilingi 10,000/= na isiyozidi shilingi 50,000/= pamoja na kulipa gharama za uharibifu wa chau.*

*Marufuku kuchukua chombo au zana ya uvuvi bila ya ruhusa*

16. (1) Ni marufuku kwa mtu yoyote kuchukua chombo au zana yoyote ndani ya chombo bila ya ruhusa ya mhusika.

*(2) Mtu yeyote atakae kiuka amri ya kifungu hiki na akipatikana na hatia atatozwa faini si chini ya shilingi 10,000/= na isiyozidi shilingi 100,000/=.*

*Marufuku kutumia chombo cha uvuvi kwa kazi isiyo ya uvuvi*

17. (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kutumia chombo cha uvuvi kwa kazi nyengine yoyote isiyokuwa ya uvuvi kwenye eneo la hifadhi bila ya dharura maalumu iliyokubalika na kijiji.

*(2) Mtu yeyote atakae kiuka amri ya kifungu hiki na akipatikana na hatia sheria za idara husika zitatumika.*

*Marufuku kukaa dago bila ya ruhusa*

18. (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kukaa dago katika vijiji au visiwa vya eneo la hifadhi wakati dago limefungwa.

(2) *Mtu yeyote atakae kiuka amri ya kifungu hiki na akipatikana na hatia atatozwa faini si chini ya shilingi 50,000/= na isiyozidi shilingi 100,000/= pamoja na kurejea anakotoka.*

*Marufuku kwenda dago bila ya kibali*

19. (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kwenda dago bila ya kuwa na kibali halali cha dago kilichotolewa na kamati ya uvuvi na kuthibitishwa na sheha wa kijiji alichotoka mvuvi.

(2) *Mtu yeyote atakae kiuka amri ya kifungu hiki na akipatikana na hatia atatozwa faini si chini ya shilingi 50,000/= na isiyozidi shilingi 100,000/= pamoja na kurejea anakotoka.*

**SEHEMU YA TATU: MAJUKUMU YA KAMATI ZA UVUVI KILA KIJIJI**

*Taratibu za utekelezaji wa adhabu kwa mujibu wa sheria hizi*

20. Kamati ya uvuvi ya eneo ndiyo itakayo simamia utekelezaji wa sheria hizi ndogo ndogo pamoja na uongozi wa Shehia (Sheha) wa kila kijiji pamoja na wananchi wote katika eneo la hifadhi.

21. Kamati ya uvuvi ya eneo katika kila kijiji husika ndiyo itakayo sikiliza malalamiko yote ya ukiukwaji wa sheria hizi, isipokuwa kwa makosa yaliyoainishiwa pahala pa kutatuliwa au kusikilizwa.

22. Kamati ya uvuvi ya eneo katika kijiji husika ndiyo itakayopokea faini zote pamoja na fidia za gharama zilizotolewa kwa makosa yaliyoanishiwa kusikiliza.

23. Faini zote zitakazotozwa kwa mujibu wa vifungu ambavyo kamati ya uvuvi ya eneo ya kijiji husika imepewa mamlaka ya kusikiliza malalamiko yake zitaingia katika mfuko wa kamati hiyo. Kwa faini zile ambazo zinahusisha watendewa makosa zitagawiwa kwa utaratibu wa asilimia 15 kwenda kwa mfuko wa kamati na asilimia 85 kwenda kwa mtendewa kosa.

24. Fidia zote za gharama zilizotozwa zitapokelewa na kamati na kuwasilishwa kwa mtendewa kosa bila kupunguzwa.

25. Mgao wote anaostahiki kupatiwa mtendewa kosa baada ya kupokelewa na Kamati ya uvuvi ya eneo katika kijiji husika zitawasilishwa kwa mtendewa kosa si zaidi ya siku tatu baada ya kamati kupokea mgao huo.

26. Ulipaji wa faini utakuwa kama ifuatavyo:-

(a) Kwa faini isiopungua shilingi. 10,000/- na isiyozidi shilingi 50,000/- italipwa kwa muda usiozidi wiki mbili kuanzia siku ambayo kamati husika imetoa maamuzi.

(b) Kwa faini isiyopungua shilingi 51,000/- na isiyozidi shilingi 100,000/- italipwa kwa muda usiozidi mwezi mmoja kuanzia siku ambayo kamati husika imetoa maamuzi.

(c) Kwa faini isiyopungua shilingi 101,000/- na isiyozidi shilingi 500,000/- italipwa kwa muda usiozidi miezi miwili kuanzia siku ambayo kamati husika imetoa maamuzi.

27. Adhabu kwa kosa lililoainishwa kusikilizwa na kuamuliwa na kamati ya eneo katika kijiji husika endapo halikutekezwa kwa sababu yoyote ile katika muda unaotakiwa shauri lake litapelekwa kwa Mkurugenzi kwa hatua zaidi.

*Uwezo wa mkurgenzi wa kufanya marekebisho ya sheria hizi*

28. (1) Mabadiliko yoyote yanayooneka yanafaa katika sheria hizi kwa lengo la kuboresha kazi za usimamizi wa shughuli za uvuvi katika eneo la hifadhi yatafanywa na Mkurugenzi.

(2) Mabadiliko yatakayofanywa yatatumika katika kipindi cha mwezi mmoja kuanzia siku ambayo Mkurugenzi na wajumbe wa kamati tendaji za maeneo ya hifadhi wamekutana kujadili na kukubaliana juu ya mabadiliko hayo.